

Watu wazima wa kuaminika hutenda vipi?



- Mtu mzima wa kuaminika ni yule ambaye maneno na matendo yake yanakufanya ujisikie salama. Watu wazima wa kuaminika...

Hu kusikiliza bila kuhukumu au kukatiza;

Hu kuamini na kuchukua wasiwasi wako kwa uzito;

Huheshimu mipaka yako, mwili wako, na nafasi yako binafsi;

Hueleza mambo kwa uwazi, ikiwa ni pamoja na kile wanachoweza na wasichoweza kuweka siri;

- Watu wazima wa kuaminika wanapaswa kutenda hivi katika maisha halisi na pia kwenye mtandao.

Watu wazima wa kuaminika HAWAPASHWI kutenda vipi?



- Watu wazima wa kuaminika **HAWATAKI** ufanye jambo lolote linalokufanya ujisikie vibaya au usalama wako uwe hatarini.

- Ha wa kutukani.

- Ha wa kuogopeshi.

- Ha wa kuumize.

Maswali ya kawaida

Kama ninahitaji msaada, namna gani nitaweza ambia mtu mzima mwenyi kuaminika?

Omba uongeye **kwenyi fasi ya upekee**. Fasiria shida zako kwa mtu mzima mwenyi kuaminika.

Ikiwa hupendi kuzungumza ana kwa ana, tuma **ujumbe wa maandishi**, tuma **barua pepe**, au andika **barua** na umpe mtu mzima wa kuaminika.

Je, itakuwaje ikiwa mtu huyo hataniamini ninaposema ninahitaji msaada?

Unastahili msaada. Ikiwa hali hii itatokea, ni sawa kuzungumza na mtu mzima mwingine ambaye kazi yake ni kukusaidia, kama vile mwalimu, msimamizi wa kesi, au mshauri. Unaweza kuwaambia watu wengi kadiri unavyohitaji mpaka upate msaada.





Watu wazima ambao kazi yao ni kuhakikisha uko salama na unapata msaada

- Wafanyakazi wa kijamii na wasimamizi wa kesi *
- Walimu, wakuu wa shule, na wafanyakazi wengine wa shule *
- Maafisa wa utekelezaji wa sheria, kama vile maafisa wa polisi *
- Madaktari, wauguzi, na wafanyakazi wengine wa afya *
- Washauri, wataalamu wa ushauri, na wataalamu wengine wa afya ya akili *

Watu wazima wa kuaminika katika jamii yako

Hawa ni watu wazima unaoweza kuwafahamu kupitia familia yako, mtaa wako, shule, michezo, jumuiya ya imani, au shughuli nyingine.

- Watu wazima katika familia yako
- Majirani
- Makocha
- Watu wazima katika mahali pa ibada
- Watu wazima katika familia za marafiki zako



Je, unapaswa kuwaamini moja kwa moja watu wazima hawa wote?



Si kila wakati. Mtu mzima wa kuaminika ni yule anayekufanya ujisikie salama, anakusikiliza, na anaheshimu mipaka yako. Imani hujengwa polepole kwa muda, na ni sawa ikiwa humwamini mtu mara moja, au hata kamwe.

Tumia orodha ya watu wazima hapo juu kufikiria kuhusu watu wazima unaowaamini katika maisha yako mwenyewe.

* Watu wazima wamoja wanatakiwa na sheria kusaidia kulinda usalama wa vijana. Watu wazima hawa wanaitwa **watu waliopewa jukumu la kuripoti matukio kwa mujibu wa sheria**. Hii ina maana kwamba ikiwa utamwambia mtu aliyepewa jukumu la kuripoti kuhusu madhara makubwa, unyanyasaji, au hatari unayopitia, anatakiwa kisheria kushiriki taarifa hiyo ili kukulinda.